**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**------------------------**

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

# TAARIFA YA THBUB WAKATI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA AFRIKA KUHUSU WATU WANAOSHIKILIWA VIZUIZINI KABLA YA KUFIKISHWA MAHAKAMANI

Aprili, 2023

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Mtaa wa Nyerere
Ploti Na. 339, Kilimani
S.L.P 1049, DODOMA
Tanzania

Simu: +255 734 047 775
+255 734 119 978
Barua pepe: info@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

*Mhe, Jaji Mfawidhi, Mahakama Kuu Dodoma;*

*Ndugu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;*

*Ndugu, Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi;*

*Ndugu, Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria;*

*Ndugu, Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum;*

*Wahe. Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;*

*Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Mashtaka Tanzania;*

*Ndugu, Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi Tanzania;*

*Ndugu,Katibu Mtendaji Tume ya Kurekebisha Sheria;*

*Ndugu, Mwakilishi wa Kamishna Jerali wa Magereza;*

*Mkuu wa Gereza, Gereza Kuu la Isanga;*

*Ndugu, Kamishna wa Sheria, Idara ya Uhamiaji Tanzania;*

*Ndugu,  Mwenyekiti wa Mawakili Dodoma, Chama cha Wanasheria Tanganyika;*

*Ndugu, Wakuu wa Idara kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;*

*Ndugu, Watumishi w Gereza la Isanga Dodoma*

*Ndugu, Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;*

*Waandishi wa habari;*

*Mabibi na Mabwana.*

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

## 1.0 UTANGULIZI

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inaungana na wadau wote barani Afrika kuadhimisha Siku ya Watu Wanaoshikiliwa Vizuizini Kabla ya Kufikishwa Mahakamani, inayoadhimishwa **Tarehe 25 Aprili** ya kila mwaka. Siku hii inatokana na Mwongozo wa Afrika kuhusu Masharti ya Ukamataji, Ulinzi chini ya Polisi na Kushikilia Watu Vizuizini kabla ya kufikishwa Mahakamani, yaani, **The Guidelines on Conditions of Arrest, Police Custody and Pre-Trial Detention**, uliopitishwa na Tume ya Haki za Binadamu na Watu Jijini Luanda, nchini Angola mwaka 2014 katika Kikao chake cha 55.

Ibara ya 45(1) ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981 inatoa mamlaka kwa Tume ya Afrika kutengeneza Kanuni au Miongozo kwa ajili ya kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na watu katika muktadha anuai.

Mamlaka za dola ndizo zenye wajibu kwa kupitia mfumo wa haki jinai kuwakamata watuhumiwa, kuwaweka mahabusu na kusimamia mchakato wote wa mfumo wa haki jinai. Kwa msingi huo mfumo wote wa haki jinai unapaswa kutekelezwa kitaalamu na kwa kuzingatia sheria na haki za binadamu. Kwa kuzingatia mfumo wa haki jinai inategemewa kuwepo kwa watu ambao watakinzana na sheria za nchi kwa hiyo inategemewa pia watu wa aina hiyo watakamatwa kwa madhumuni ya kufikishwa katika vyombo vya sheria ili haki iweze kupatikana. Maswali ambayo tunaweza kujiuliza ni iwapo mtu atapaswa kukamatwa, je nguvu inayotumika kumshika iko sawa?, na je katika kumshika dhana ya uwajibikaji inatumika?

Ni muhimu sana kwa vyombo vinavyotekeleza mfumo jinai wakati wa utekelezaji wake kujiuliza maswali haya kwa kuwa, Sheria zote za Kimataifa, Kikanda na hata za nchi zinatambua kuwa ni marufuku kwa mtu yeyote aliyeshitakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo.[1]

Kulingana na sheria zilizotajwa hapo juu, Serikali na Mamlaka zake zimepewa jukumu la kulinda, kuheshimu, na kutekeleza haki za binadamu zikiwemo haki za mahabusu na wafungwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

Mwongozo wa Luanda ulitolewa kwa sababu nchi nyingi duniani haswa za Afrika zilionekana kuwa na mlundikano wa watu kwenye Magereza na kitakwimu idadi kubwa ya watu hao ilikuwa ni ya mahabusu zaidi ya wafungwa. Ilibainika kuwa baadhi ya mahabusu walikaa katika vituo vya Polisi kwa muda mrefu kinyume na taratibu na Sheria za nchi. Aidha, ilibainika pia kuwa mahabusu wengine waliteswa na kudhalilishwa wakati wanahojiwa na Polisi, wengine walikaa mahabusu kwa muda mrefu hata bila ndugu zao kujulishwa au kujua waliko, wengine hawakupewa nafasi ya kuwasiliana na wanasheria au ndugu zao. Wengine walikosa huduma za afya na wengine hawakujulishwa haki zao wanapokuwa mikononi mwa Polisi.[2]

Ilibainika pia kuwa Watuhumiwa pia wanapokaa mahabusu kwa muda mrefu wanakumbana na changamoto ya kupoteza ajira na

[1] Ibara ya 13(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Sura ya 2.

[2] Justice initiative.org/voice/raising-profile-pretrial-detention-Africa, 7:22Mchana 27/4/2023; pia Taarifa zote za THBUB za Ukaguzi wa Magereza kwa upande wa Tanzania..

familia zao, wanapoteza heshima na utu wao kwenye jamii. Wengine wameingia mikataba ya kukukubali kutenda makosa (plea bargaining) ili tu kuachiwa huru kwa ajili ya kulinda utu, kazi zao na familia zao.

## 1.1 Chimbuko na lengo la Mwongozo wa Luanda

Kabla ya Mwongozo wa Luanda kuhusu watu wanaozuiliwa kutokana na changamoto za kijinai kumekuwepo hatua mbalimbali kama vile Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kuanzisha Msimamizi Maalumu wa Masuala ya Ukamataji na Uhifadhi wa Watuhumiwa na Hali za Magereza (Special Rapporteurship on Prisons and Conditions of Detention in Africa) mwaka 1996 na baadaye kufuatiwa na Tamko la Kampala kuhusu Hali ya Magereza Afrika (The Kampala Declaration on Prisons Condition in Africa of 1996).

Mwaka 2002 Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu iliridhia Mwongozo wa Kisiwa cha Robben (The Robben Island Guidelines) ambao kimsingi ulizishauri Serikali za Afrika kuridhia vigezo vya kimataifa kwenye uimarishaji wa hali za magereza kwenye nchi husika. Baada ya Mwaka Tume ya Afrika tena iliridhia uwepo wa Ouagadougou Declaration and Plan of Action on Accelerating Prison and Penal Reform in Africa. Masuala yaliyozungumziwa ni pamoja na hali za Magereza Afrika, kupunguza idadi ya wafungwa, wajibu wa Azaki hali ya magereza na namna ya kuwahudumia wafungwa, Usimamizi mzuri wa magereza na namna ya kujiwezesha kihuduma, adhabu mbadala ikiwemo huduma kwa Jamii, kupunguza idadi ya mahabusu, haki za watoto magerezani, na mchanganyiko wa namna mbalimbali ya

mfumo wa haki jinani na utoaji wa adhabu kwa mazingira ya Afrika.[3]

Mwongozo wa Luanda uliendeleza na kusisitiza uzingatiwaji wa Ibara za 2, 3, 5, 6 na 7 za Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, ambazo zinataka nchi wanachama kutekeleza majukumu ya kuhakikisha kuwa haki za kuishi, utu, ulinzi na usawa, usawa mbele ya sheria na uhuru wa mahakama zinazingatiwa na nchi wanachama katika mnyororo mzima wa haki jinai kabla ya hukumu.

Hivyo, Mwongozo wa Luanda umelenga kuhakikisha kuwa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zilizoridhia Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, zinaimarisha mifumo yao ya Haki Jinai ili kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inaheshimu na kuzingatia viwango stahiki vya haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

## 1.2 Maeneo yanayoguswa katika Mwongozo wa Luanda

i) **Ukamataji**: Kuzingatia haki za watuhumiwa, ikiwa ni pamoja na kuwaeleza sababu za kukamatwa kwao na kuwaelezea haki zao za msingi wakati wameshikiliwa;

ii) **Uhifadhi chini ya ulinzi wa Polisi**: Kuhakikisha kuwa matumizi ya nguvu kwa upande wa polisi yanazingatia viwango vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria; watuhumiwa wanapewa msaada wa kisheria na dhamana; na mahojiano yanafuata taratibu zilizowekwa kisheria;

[3] Southernafricalitigationcentre.org/wp-content/uploads/2017/03/Ouagadougou-Declar.pdf, 8;29 Mchana, 27/04/2023

iii) **Rejesta (*Registers*)**: Rejesta kuzingatia misingi ya uwazi na zinabainisha taarifa sahihi na za kweli kuhusu watuhumiwa ambazo zinaweza kupatikana muda wowote;

iv) **Vifo au kujeruhiwa chini ya ulinzi wa Polisi**: Kuchukua hatua zinazopaswa pale mtuhumiwa anapojeruhiwa, au kupoteza maisha mikononi mwa polisi, au chombo kingine cha dola, ikiwa ni kuhakikisha kuwa mtuhumiwa anapata matibabu na uchunguzi huru wa vifo;

v) **Mazingira ya mahali watu wanamoshikiliwa**: Mwongozo umeonesha haja ya watu kuwekwa mahala salama na kutenganishwa kutokana na mahitaji yao kwa kuzingatia umri, hali ya afya, na jinsia;

vi) **Makundi maalum**: Mwongozo umeainisha makundi ya watu yaliyotajwa kwenye Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (akina mama, watoto, wenye ulemavu, na wasio raia) na haja ya makundi hayo kuhudumiwa kwa utaratibu maalumu;

vii) **Wajibu wa maafisa na fidia kwa wahanga**: Mwongozo umeonesha haja ya kuwepo kwa utaratibu wa ukusanyaji taarifa, usimamizi, uchunguzi, ukaguzi, utaratibu wa kuwasilisha malalamiko, madai ya fidia dhidi ya wanaowashikilia watuhumiwa kwa mujibu wa sheria pale ambapo haki za watuhumiwa hao zinavunjwa.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA LUANDA

**i)** Wadau wote wa haki za binadamu kikanda na kitaifa, wana jukumu la kutekeleza Mwongozo huu. Tume ya Afrika ambayo, kwa mfano, ina jukumu la kuhakikisha kuwa uzingatiwaji wa Mwongozo huu na kufuatilia hatua za mwongozo huo kwa nchi wanachama, na kuwezesha utekelezaji wake kwa kushauri ipasavyo.

**ii)** Serikali za nchi wanachama wana jukumu la kutekeleza Mwongozo huu kwa kuboresha sheria, sera na namna Taasisi zake za Haki Jinai zinavyotekeleza majukumu yao sanjari na yaliyoainishwa kwenye Mwongozo uliotajwa. Mabunge ya nchi wanachama wana jukumu la kutekeleza Mwongozo huu kwa kuboresha Sheria anuai sanjari na Mwongozo huu na pia kwa kuhoji mifumo na Taasisi za Haki Jinai pale inapokwenda kinyume na Mwongozo wa Luanda.

**iii)** Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu za Nchi (National Human Rights Institutions – NHRIs), kama ilivyo THBUB, zina jukumu la kuhamasisha, kutoa elimu, kuchunguza, na kutoa mapendekezo kwa Taasisi za Haki Jinai juu ya namna ya kuboresha utendaji kazi wao sanjari na Mwongozo tajwa. Na mwisho, AZAKI zina jukumu la kutekeleza Mwongozo huu kwa kupiga kelele na kutoa ushauri pale ambapo inastahili.

## 3.0 HAKI JINAI KAMA HAKI ZA BINADAMU NCHINI TANZANIA

Msingi wa haki jinai unatokana na haki ya usawa mbele ya sheria inayoelezwa katika ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania, 1977 ambayo inaelezea usawa mbele ya sheria kwa watu wote na kwamba haki na wajibu wao utalindwa na kuamuliwa na mahakama na vyombo vilivyowekwa na sheria. Katika kuhakikisha usawa huo, ibara ya 13 (6) inasisitiza uwepo wa haki ya kusikilizwa na rufaa, dhana ya kutokuwa na hatia mpaka ithibitishwe, kupewa adhabu kwa mujibu wa sheria, heshima ya mtu kutunzwa wakati wa upelelezi na katika hatua zote pamoja na mtu kutoteswa na kupewa adhabu za kutweza na kudhalilisha.

Hapa nchini, pamoja na Katiba, kuna sheria mbalimbali zinazosimamia haki jinai ikiwemo Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291; Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6; Sheria ya Uangalizi wa Wahalifu, Sura ya 247; Sheria ya Bodi ya Msamaha kwa Wafungwa, Sura ya 400; Sheria ya Magereza, Sura ya 58; Sheria ya Mtoto, Sura ya 13; Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura ya 322; Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16; Sheria ya Mahakimu, Sura ya 11; Sheria ya Kiwango cha Chini cha Adhabu, Sura ya 90; Sheria ya Taifa ya Uendeshaji Mashtaka, Sura ya 430; Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Na. 11 ya 2007; Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200; Sheria ya Ugaidi, Na. 21 ya 2002; *The Age of Majority Act, Cap* 43; Sheria ya Ndoa 1971, Sura ya 29; *The Corporal Punishment Act, Cap* 17; *Discharge of Duties Act, No. 14 of 2005*; Sheria ya Madawa ya Kulevya, 2015; Sheria ya Uangalizi wa Wahalifu, Sura ya 247; Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287; pamoja na sheria nyingine zinazohusiana kama vile Sheria ya Eneo la Uhifadhi Ngorongoro, Sura ya 413.

## 3.1 Mnyororo wa Haki Jinai

Haki Jinai ni mchakato wa utoaji haki kwa waliofanya makosa ya jinai au wanaoshutumiwa kufanya makosa hayo. Mchakato huu wa haki jinai una mnyororo mrefu ambao unaanzia tangu *kuzuia uhalifu, kubaini uhalifu, ukamataji, upelelezi, uendeshaji wa mashtaka, usikilizwaji wa kesi, haki ya uwakilishwaji na utetezi, utoaji wa vifungo, urekebishaji wa wafungwa, usimamizi na urekebu*.

## 3.2 Changamoto katika Usimamizi wa Haki Jinai

THBUB inatambua juhudi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyombo vyake katika kuimarisha mfumo wa haki jinai. THBUB imekuwa ikifuatilia usimamizi wa haki jinai katika utekelezaji wa majukumu yake. THBUB imekuwa ikipokea malalamiko, kufanya ziara katika magereza na sehemu wanamozuiliwa watu na kufanya chunguzi mbalimbali zinazohusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Kupitia kazi hizo, THBUB imebaini kuwepo changamoto kadhaa katika usimamizi wa haki jinai nchini. Changamoto hizo zimegawanyika katika maeneo mbalimbali yakiwemo masuala ya kisheria, kimuundo, masuala ya utendaji/utumishi, miundo mbinu na maeneo mengine ambayo kwa namna moja au nyingine yanagusa mfumo wa haki jinai. Maeneo haya yameonekana kugusa vipengele vyote vya mnyororo wa haki jinai. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo:

### 3.2.1 Ukamataji wa Watuhumiwa na upelelezi wa makosa ya jinai

Ukamataji wa watuhumiwa na upelelezi wa makosa ya jinai unafanywa na Polisi na vyombo vingine vilivyopewa mamlaka hayo. Katika eneo hili, THBUB imebaini changamoto zifuatazo:

i) **Udhaifu na kuchelewesha upelelezi**

ii) **Matumizi ya nguvu wakati wa ukamataji na mahojiano**

iii) **Watuhumiwa kukaa mahabusu muda mrefu**

### 3.2.2 Haki ya kupata dhamana

THBUB imebaini ongezeko la idadi ya makosa yasiyokuwa na dhamana katika sheria mbalimbali zinazotungwa. Sheria hizo ni: Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20, kifungu cha 148(5) ambacho kimeorodhesha makosa mbalimbali ambayo hayana dhamana, yakiwemo; mauaji, uhaini, ujambazi wa kutumia silaha au unajisi wa mtoto, makosa mengine ya kumiliki na kusafirisha madawa ya kulevya yanayozidi kiasi cha shilingi milioni kumi(10,000,000/=) chini ya Sheria ya Kupambana na Kudhibiti Madawa ya Kulevya ya Mwaka 2015, ugaidi chini ya sheria ya Kuzuia Ugaidi Sura ya 19 ya mwaka 2002, na makosa baadhi ya uhujumu uchumi chini ya Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200. Aidha, katika ziara za THBUB katika magereza baadhi ya mahabusu walilalamikia masharti magumu ya dhamana, hali iliyowafanya kushindwa kutimiza masharti hayo, hivyo kuendelea kuwepo gerezani.[4]

Ni maoni ya Tume kuwa badala ya kuongezeka kwa makosa yasiyo na dhamana kwa mujibu wa sheria yanaminya haki za

[4] Taarifa ya Magereza katika Gereza la Isanga, Msalato na Kondoa

watuhumiwa kwa mujibu wa Ibara ya 13(6) ya Katiba ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jukumu hili lingeachiwa mahakama ambayo inaweza kutoa dhamana au kukataa kwa kuzingatia mazingira ya kila kosa. Pengine makosa yasiyo na dhamana yangebakia kuwa machache.

## 4.0 TAKWIMU ZA WATU WANAOZUILIWA KUSUBIRI KESI KUSIKILIZWA

Takwimu zilizopo zinabainishi kuwa jumla ya watu 11,580 wamezuiliwa na Idara ya Uhamiaji, Tume ya Madwa ya Kulevya na Magerezani Tanzania Bara. Takwimu hizi hazijumuishi watu waliozuiliwa katika selo za Polisi na taasisi nyingine zinazozuia watu kwa mujibu wa Sheria. Mchanganuo wa takwimu tajwa hapo juu ni kama zinavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini.

| **Idadi ya Mahabusu** | | **Idadi ya Watoto wanao kinzana na sheria** | | **Idadi ya Wagonjwa wa afya ya akili** | | **Idadi ya Watu wenye ulemavu** | | **Idadi ya raia wa kigeni** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Me** | **Ke** | **Me** | **Ke** | **Me** | **Ke** | **Me** | **Ke** | **Me** | **Ke** |
| 10285 | 477 | 156 | 07 | 83 | 07 | 39 | 02 | 524 | 24 |

**Chanzo:** Jeshi la Magereza, Idara ya Uhamiaji na Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya kwa Mwezi Aprili, 2023.

Jedwali hapo juu linaonesha kwamba idadi ya Wanaume wanaozuiliwa ni 11,087, wanawake 510, Watoto 163 wakiwemo watoto wa kike saba (7). Hata hivyo, takwimu hizo zinaonesha kuna raia wa kigeni 548 waliozuiliwa kwa tuhuma za makosa ya uhamiaji, madawa ya kulevya na makosa mengine ya jinai.

## 5.0 PONGEZI KWA SERIKALI

Wakati tukiadhimisha siku hii, Tume inapenda kuipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali za kufanya marekebisho, ikiwemo kufanya marekebisho ya Sheria za Haki za Jinai na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuunda Tume ya kushughulikia Mfumo wa Haki Jinai. Pia ni Serikali yetu kwa kushirikiana na Tume ya Afrika pamoja na wadau wengine walitafsiri Mwongozo huu kwa lugha ya Kiswahili, mwaka 2017, na hivyo kurahisisha uelewa wa Mwongozo huu kwa Taasisi za Haki Jinai nchini na wananchi kwa ujumla.

## 6.0 HITIMISHO

THBUB inatambua uwepo wa Tume ya Haki Jinai iliyoundwa na Mhe. Rais, Samia Suluhu Hassan kwa lengo la kupitia Mfumo Mzima wa Haki Jinai na kupendekeza maboresho. Tunategemea maboresho yatakayofanyika yatasaidia katika kuimarisha mfumo wa haki jinai kwa kupunguza au kuondoa kabisa changamoto za walio vizuizini kutokana na changamoto za kisheria. Aidha, kama ilivyoelezwa hapo awali kuwa jukumu la kutekeleza Mwongozo wa Luanda kwa manufaa ya nchi yetu ni la wadau wote, hivyo ni imani ya THBUB kuwa wadau wote watatoa maoni yao na kuyawasilisha kwenye Tume husika ambayo itapendekeza kwa serikali maboresho ambayo yatazingatia pia Mwongozo wa Luanda.

THBUB kwa kutambua umuhimu wa kukumbushana wajibu wa kila mdau kwenye sekta ya haki jinai, itaendelea kuadhimisha siku hii kila mwaka ifikapo Tarehe 25 Aprili.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Mathew P.M. Mwaimu (Jaji Mst.)

**Mwenyekiti**

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

28 Aprili, 2023